



TAARIFA KWA UMMA

Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) linakanusha taarifa inayosambazwa katika mitandao ya Kijamii ikionesha gharama mbalimbali anazotakiwa kulipia Kijana aliyechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2022.

Taarifa hiyo imetolewa katika Taarifa kwa Umma ya wito wa kujiunga na Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2022 iliyotolewa na Makao Makuu ya JKT tarehe 31 Mei 2022.

Katika taarifa hiyo **Fake** imeongezwa gharama za Vifaa vilivyoainishwa katika taarifa halisi ya JKT pamoja na gharama za fedha za Mafunzo anazotakiwa kulipia Mwanafunzi kupitia akaunti namba za Makambi husika anayokwenda Kijana.

JKT linapenda kuutarifu Umma kuwa, Taarifa hiyo ni ya Uongo na siyo iliyotolewa na Makao Makuu ya JKT Tarehe 31 Mei 2022 hivyo linawataka wananchi kuipuuza.

Vile vile JKT linapenda kuwataarifu wananchi kuwa Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria na yale ya kujitolea yamelenga kumjengea Kijana wa Kitanzania Ukakamavu, Nidhamu, Uzalendo na kuleta Umoja wa Kitaifa, Hivyo Mafunzo hayo yanatolewa na Jeshi hilo bila kijana kulipia gharama yoyote, Vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo Makambini wanatoka navyo majumbani mwao.

Jeshi la Kujenga Taifa, Linatoa onyo kwa mtu yoyote aliyehusika kupotosha umma wa Watanzania, Tayari uchunguzi wa kubaini muhusika wa kutunga na kusambaza taarifa hizo kwa namna yoyote ile unaendelea, Atakayebainika atachukuliwa hatua za Kisheria mara moja.

Aidha, Jeshi la Kujenga Taifa linawasisitiza vijana kuendelea kuripoti Makambini wakiwa na vifaa vilivyoainishwa katika tovuti ya JKT ambayo ni www.jkt.go.tz

**Imetolewa na:
Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,
Makao Makuu ya JKT,
Tarehe 07 Juni 2022.**

